



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

MKURUGENZI MKUU LATRA ATOA POLE KWA MKUU WA MKOA WA TANGA

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, CPA Habibu Suluo, ametoa salamu za pole kwa Mhe. Omary Tebweta Mgumba, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, kufuatia vifo vya watu 17 na majeruhi 12 vilivyotokana na ajali iliyotokea Ijumaa, tarehe 3 Februari, 2023 saa 4:22 usiku eneo la Magila Gereza, tarafa ya Mombo Wilayani Korogwe mkoani Tanga.

Ajali hiyo ilihusisha gari la mizigo aina ya Mitsubishi Fuso lenye namba za usajili T673 CUC na gari la abiria aina ya Coaster lenye namba za usajili T863 DXN iliyokuwa imebeba mwili wa marehemu, familia na ndugu wa marehemu waliokuwa wakisafiri kutoka Dar es Salaam, kuelekea Rombo, mkoani Kilimanjaro.

Katika salamu zake, CPA Suluo ametoa pia pole kwa familia, ndugu, jamaa na wafiwa wote; vilevile amewapa pole majeruhi na kuwaombea uponaji wa haraka.

Mfumo wa LATRA wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) unaonesha kuwa gari hilo la abiria lilitoka Dar es Salaam maeneo ya Mbezi Luis tarehe 3 Februari, 2023 saa 8:07 mchana, na lilipata ajali hiyo lilipofika Korogwe. LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani watafanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha ajali hiyo na kuchukua hatua stahiki za kuzuia ajali za aina hii.

Aidha, LATRA inawakumbusha madereva wote wa vyombo vya usafiri kibiashara kufika ofisi za LATRA katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ili kusajiliwa na hatimaye kuthibitishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 na Kanuni za Usajili wa Wahudumu na Uthibitishaji wa Madereva za mwaka 2020.

Kwa taratibu za LATRA, madereva wote wa magari maalum ya kukodi (Special Hire) hawaruhusiwi kuendesha magari hayo bila kusajiliwa na kuthibitishwa na LATRA.

Imetolewa na:
Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano – LATRA
04 Februari, 2023